

HALMASHAURI YA MANISPAA MPANDA



TAARIFA YA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI HALMASHAURI YA MANISPAA MPANDA - TASAF III KUANZIA APRILI 2014 HADI APRILI 2018:

1:0 UTANGULIZI:

Awamu ya tatu ya Mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF III) inayotekeleza Mpango wa kunusuru kaya maskini ilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe.Dkt.Jakaya Mrisho Kikwete mwezi Agosti mwaka 2012.Katika Halmashauri ya Mji wa Mpanda mpango huu ulizinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi mhe. Dk. Rajabu Rutengwe mnamo tarehe 8, Aprili 2014 katika ukumbi wa Idara ya Maji Halmashauri ya Wilaya Mpanda, ambapo ilifuatiwa na Warsha Maalum kwa Wadau wote wa Mpango huu katika Halmashauri ya Mji na kuongozwa na Timu kutoka TASAF Makao Makuu (TMU).

Lengo kuu la mpango huu ni kuiwezesha jamii kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi.

2:0 UTEKELEZAJI WA MPANGO:

Mpango wa kunusuru kaya maskini unalenga kutekelezwa katika nyanja zifuatazo;

- 1: Uhawilishaji wa fedha katika kaya maskini(Utoaji wa fedha ya ruzuku isiyo na masharti na yenye masharti katika kaya maskini)
- 2: Utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya miundo mbinu 'Targeted Infrastructure'
- 3:Utekelezaji wa miradi ya ajira za muda mfupi hasa katika kipindi cha hari
- 4: Utekelezaji wa mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya.

2:1: RUZUKU KWA KAYA MASKINI :

Mpango wa kunusuru kaya maskini unaenda sambamba na utoaji wa ruzuku kwenye kaya hizo, kila baada ya miezi miwili;ruzuku zinazotolewa ni za aina mbili, ambazo ni:

- 1: Ruzuku ya kawaida kwa kaya zote maskini zilizotambuliwa na kuandikishwa .



Mkutano wa kijamii katika kijiji cha Mbugani kabla ya kuanza uhawilishaji wa fedha ambapo walengwa wanakumbushwa kutumizia vizuri fedha wanapokea.



Malipo ya walengwa katika Mtaa wa Kachoma.

2: Ruzuku ya masharti ya:

- ✓ Afya kwa kaya zenye Watoto chini ya umri wa miaka mitano pamoja na wanawake wajawazito.
- ✓ watoto wenye umri wa kwenda shule.

Zoezi la uandikishaji wa kaya Maskini liliambatana na usajili wa Watoto walio katika kaya wanao takiwa kutimiza masharti ya Elimu na Afya. Jumla ya Watoto wa kutimiza masharti ya Elimu ni Watoto 1208 na Masharti ya Afya ni watoto 679.

2:2 MIRADI YA MAENDELEO YA MIUNDO MBINU (INFRASTRUCTURE DEVELOPMENT)

Miradi ya Maendeleo ya Miundo Mbinu (Infrastructure Development) ; mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Mlima Kipala, Kijiji cha Mwamkulu fedha zililetwa **TSHs 72,978,444.00** hadi sasa, fedha hizi zimetumika katika ujenzi, na Kamati ya usimamizi wa ujenzi ilikabidhi jengo baada ya kukamilika tayari kwa kuanza kutoa huduma tangu tarehe **02/02/2018**. Lengo ni kusogeza huduma kwa walengwa na jamii kwa ujumla katika kuimarisha rasimali watu katika jamii.



Zahanati ya Mlima Kipala katika kijiji cha Mwamkulu.





Samani za Zahanati ya Mlima Kiapala zikipangwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya usimamizi wa ujenzi wa zahanati.

2:3 Utekelezaji wa ajira za muda mfupi kwa walengwa

Utekelezaji wa miradi ya ajira za muda mfupi hutekelezwa na walengwa wanaonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini, kwa lengo la kujipatia kipato kipindi cha hari (hali ngumu), kama ilivyo kwa walengwa wengine walio katika halmashauri zilizo katika mpango wa kunusuru kaya maskini nchini.

Ajira za muda hutolewa kwa wanaohiari kufanya kazi katika kipindi cha miezi 4, kwa kila mwezi siku 15, na hufanyika katika kipindi cha mwezi Septemba hadi Desemba, na kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ajira hizi zitatekelezwa kuanzia Agosti hadi Novemba.

Pamoja na kuwapatia walengwa fursa ya kupata kipato, malengo mengine ni kutengeneza rasimali za jamii katika mitaa na vijiji vinavyotekeleza miradi hii kwa manufaa ya jamii nzima, na kuwajengea uwezo walengwa kupata maarifa ya kumudu mazingira kwa kutumia teknolojia rahisi na rasimali zinazowazunguka kuboresha maisha.

2:4: Utekelezaji wa mpago wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya.

Hiki ni kipengele kingine muhimu katika mpango wa kunusuru kaya maskini ambapo walengwa wanajengewa uwezo wa kujiweka akiba na kukuza uchumi wa kaya, ambapo hata baada ya mradi wa uhawilishaji fedha kwa walengwa kumazika walengwa watakuwa na uwezo wa kuendesha maisha yao na kukabili matatizo kutokana na uwekezaji utrakaofanywa kwa kupitia vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana katika kukuza uchumi wa kaya.

3:0 KUONDOA KAYA ZISIZO NA SIFA KATIKA MPANGO:

Zoezi la kuondoa kaya zisizo na sifa ni endelevu ambapo uhakiki wa mara kwa mara hufanyika kwa ajili ya kurekebisha taarifa za kaya maskini zinazostahili kuendelea

kupata ruzuku.Mojawapo ya sifa zinazoweza kuindoa kaya ni pamoja na kifo au kuhama bila taarifa yoyote, au kuingizwa kimakosa pasipo kuzingatia vigezo vinavyostahili.Hadi sasa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ina kaya za walengwa **1,501** kutoka **1,747** zilizotambuliwa na kuandikishwa tangu Septemba 2014.

4:0 KUONGEZA VIJJI NA MITAA ILIYO SAHAULIKA KUIINGIZWA KWENYE MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI;

Jumla ya vijiji **29** viliombewa kuingizwa kwenye Mpango, baada ya kufanya ufuatiliaji na kuainisha kuwa vinasifa ya kuingizwa kwenye Mpango. Orodha ilisha wasilishwa TASAF Makao makuu, kinachosubiriwa ni maelekezo ya namna gani utekelezaji utafanyika toka TASAF Makao Makuu.

Naomba kuwasilisha.